JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 24 - 2019/2020**

**DHIDI YA**

**GLOBAL PUBLISHERS AND GENERAL ENTERPRISES LIMITED**

**UAMUZI**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA MITANDAONI), 2018.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni ya kutoa huduma ya utangazaji kwa **Global TV** ili kuchapisha na kutangaza habari mbali mbali mtandaoni.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 4 ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kutunza kumbukumbu za watoa huduma wote wa maudhui mitandaoni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma za mitandaoni ye yote atakayekiuka Kanuni za Maudhui Mtandaoni au Sheria nyingine.

1.3 Tarehe 26 Februari, 2020, **Global TV** kupitia chaneli yake ya Youtube inatuhumiwa kuchapisha picha za mnato na kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha na yenye kushabikia vitendo vya mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja. Maudhui yao yanaweza kuwaumiza na kuwakwaza waumini wa dhehebu la Anglikana na jamii ya Kitanzania kwa ujumla, jambo ambalo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji.

1.4 Mtangazaji wa **Global TV** alitoa taarifa hiyo yenye ukakasi na isiyokubalika katika utamaduni wa jamii ya kitanzania bila kuzingatia Weledi na Maadili ya Utangazaji pale alipoeleza kuwa **Mchungaji John**

**Mayerepi** wa Afrika Kusini na **Mchungaji Paul Mwaura** wa Kenya, wote wa Kanisa la Anglikana wameamua kufunga ndoa baada ya kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja kwa muda mrefu. Mtangazaji huyo aliendelea kunukuu maneno yaliyosemwa na **Mchungaji John Mayerepi** kwamba amekuwa akishiriki tendo kwa muda mrefu na "mumewe" (**Mchungaji Paul Mwaura**) huku wakiungwa mkono na wenzao kutoka kundi la LGBT (Lesbian, Gay, Bisexual and Transgender).

1.5 Mtangazaji wa **Global TV** alionesha picha za mnato na kusikika akitamka maneno yafuatayo:

***"...ama kweli mambo ni mambo na vituko vinaendelea kutokea duniani, mchungaji anayejihusisha na mapenzi ya jinsia moja amefunga ndoa na mwanaume Afrika Kusini. Mchungaji wa Kanisa la Anglikani ambaye anajihusisha na mapenzi ya jinsia moja huko nchini Afrika Kusini amefunga ndoa na mpenzi wake wa kiume wa muda mrefu ambaye ni raia wa Kenya kisha kufanya party kubwa na ya kifahari nchini humo".***

***"Akizungumza mchungaji John Mayerepi amesema amekua akishiriki tendo kwa muda mrefu na "mumewe" Mchungaji Paul Mwaura huku wakiungwa mkono na wenzao kutoka LGBT. Na walipoulizwa kwa nini waliamua kuwa mashoga wahubiri hao walijibu kwamba mwelekeo wa kijinsia ni wa kuzaliwa si wa kujichagulia na usiobadilika. Kisha wakadai kuwa wasihukumiwe wala kuguswa".***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kwa kitendo cha kuchapisha picha za mnato na kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha na yenye kushabikia vitendo vya mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja, **Global TV** inatuhumiwa kukiuka Kanuni Na. 5(1) (a) na (b), 7(1) (a) na (b) na 12 (b) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018. Kanuni tajwa zinasomeka kama ifuatavyo:

*5-(1) For the purpose of these Regulations, an online content provider shall have the obligations to-*
*(a) ensure that online content is safe, secure and does not contravene the provisions of any written law;*
*(b) take into account trends and cultural sensitivities of the general public.*

*7-(1) A licencee of online radio and television intended for broadcasting over the public internet with the objective of informing, entertaining and educating the public shall adhere to the following conditions:*

*(a) content streamed to abide to regulations governing the broadcasting services;*
*(b) adhere to journalism ethics and professionalism.*

*12.-Online content services provider shall not publish-*

*(c) Obscene content.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

Tarehe 19 Juni, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia Uongozi wa **Global TV** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza kuhusu tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 24 Juni, 2020, Uongozi wa **Global TV** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Eric Shigongo**, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo. Pia, tarehe 25 Juni, 2020, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Abdallah Mrisho**, Meneja Mkuu wa **Global TV**, pamoja na **Calvin E. Nyorobi**, Msimamizi wa Kituo ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA, KUSIKILIZA NA KUANGALIA MAUDHUI YA GLOBAL TV.

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Global TV** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Global TV** walisikiliza na kuangalia maudhui yaliyochapishwa na kutangazwa na **Global TV** tarehe 26 Februari, 2020 na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

## 5.0 UTETEZI WA GLOBAL TV

Katika maelezo yao ya maandishi**, Global TV** walikiri kurusha maudhui yasiyofaa na kudai kuwa hawakuwa na nia ya kupotosha jamii wala kukiuka Kanuni. Walidai kuwa mwanzoni mwa habari hiyo, mtangazaji alisikika akikiri kwamba habari hiyo ni "vituko" na neno hilo katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Dar es Salaam (TUKI), Toleo la Mwaka 2004 linamaanisha "tukio la kushangaza, kioja, ajabu, hekaya, shani". Kwa hiyo, waliichukulia taarifa hiyo kama kituko ambacho pia kiliripotiwa na vyombo mbali mbali vya nje ya Tanzania.

Waliendelea kudai kuwa baada ya kupokea barua ya wito kutoka TCRA na kugundua kuwa kuna baadhi ya watu wamekwazika ambao hawakuwahi kutoa maoni yao kwenye habari hiyo wala kuwapigia simu ya malalamiko, waliamua kuiondoa habari mtandaoni na waliohusika walipewa barua ya onyo na kutakiwa kuongeza umakini. Waliambatanisha barua ya onyo iliyotolewa na **Calvin Nyorobi**, aliyetangaza maudhui hayo.

Walimalizia kwa kuomba radhi wakidai kuwa wamekuwa wakizingatia Weledi, Maadili ya Kitanzania na masharti ya leseni na waliahidi kuongeza umakini ili kutotenda tena kosa kama hilo.

Pia, **Global TV** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo:

5.1 **Abdallah Mrisho** alianza kwa kurudia maelezo yao ya maandishi na kisha kusema kuwa wamefanya kosa kwa bahati mbaya na hawakuwa na mtazamo walioelezwa na Kamati kwa sababu tukio hilo limetokea nje ya nchi ambapo vitendo hivyo ni vya kawaida. Alidai kuwa walihisi watazamaji wao hawatakwazika kwa sababu utamaduni huo haupo Tanzania lakini pia wanatoa rai kwa Watanzania kuhakikisha mambo hayo hayaingii nchini kwetu. Aliendelea kudai kuwa walichukua tahadhari kwa kuchuja baadhi ya vitu visivyofaa katika taarifa hiyo na kubakisha tu ambavyo Uongozi wao ulivipitisha vichapishwe, lakini kumbe bado hawakuwa sahihi.

Alipokuwa akijibu maswali ya Kamati, **Abdallah** alikiri kuwa katika maudhui yao hawakutoa maneno yo yote ya kuelimisha jamii kuwa vitendo vile ni vibaya na kuomba radhi kwa udhaifu huo waliouonesha. Alisema ametambua kuwa walitakiwa kuielimisha jamii kuwa jambo lile siyo jema na walikosea kwa kudhani kuwa habari yenyewe ilitosha kuelimisha na kutahadharisha jamii.

5.2 **Calvin E. Nyorobi** alianza kwa kuunga mkono maelezo ya **Abdallah Mrisho** na kudai kuwa walipata hamasa ya kuitangaza habari hiyo kwa sababu vyombo vingine na mitandao viliitangaza pia na havikufungiwa na Youtube. Pia, alidai kuwa waliifanyia ufuatiliaji habari hiyo kwa kuangalia maoni ya watazamaji lakini hawakuona malalamiko yo yote. Alisema kuwa hawawezi kushabikia vitu ambavyo vinaweza kuleta athari kwenye jamii.

Alipoulizwa maswali na Kamati, **Calvin** alijibu kuwa kitendo cha kuchapisha habari isiyofaa kwa kigezo cha kwamba imechapishwa na vyombo vingine haikuwa sababu sahihi kitaaluma. Pia, alijibu kuwa kutokuwepo kwa malalamiko ya watazamaji wao katika habari hiyo siyo kigezo tosha cha kuonesha kuwa maudhui waliyoyachapisha hayakuwa na kasoro.

## 6.0 MAJUMUSHO YA UTETEZI WA GLOBAL TV

Katika kujumuisha utetezi wao**, Global TV** walisema kuwa maelezo ya Kamati yamewafumbua macho, yamewaelimisha na kuwajenga. Walimaliza kwa kusema kuwa watazingatia usimamizi makini wa maudhui yao na kwamba tayari wameshatoa mwongozo mpya wa uhariri ili makosa kama hayo yasijirudie tena.

## 7.0 TATHMINI YA KAMATI

Baada ya kusikiliza utetezi wa **Global TV**, Kamati ya Maudhui inatoa tathmini ifuatayo:

7.1 **Global TV** imetenda kosa la kuchapisha picha za mnato na kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha na yenye kushabikia vitendo vya mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja kwa sababu imeonekana wazi kuwa picha hizo, maudhui na lugha waliyotumia katika kipindi chao vililenga kuihamasisha jamii kuiga vitendo vya mapenzi ya jinsia moja na sio kuelimisha jamii kuchukua tahadhari;

7.2 **Global TV** imekiuka Weledi na Maadili ya Utangazaji wa Habari kwa kuchapisha picha za mnato na maudhui ambayo hayakubaliki katika Sheria na Utamaduni wa Tanzania na ambayo yanaweza kuishawishi jamii ya Kitanzania kuiga vitendo viovu;

7.3 Kamati ya Maudhui imejiridhisha kuwa wasimamizi wa **Global TV** wameonesha udhaifu katika Uhariri wa maudhui yao kwa kitendo chao cha kuchuja kidogo maudhui yasiyofaa na kisha kuruhusu vipengele vingine vya maudhui hayo hayo kurushwa katika chaneli yao;

7.4 Kamati imebaini kuwa utetezi wa **Global TV** kuwa walirusha habari hiyo kama kituko hauna msingi kwa sababu walitakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Weledi na Maadili ya Utangazaji wa Habari kwa kutotangaza maudhui yanayokinzana na Sheria na Utamaduni wa Kitanzania. Si kila kituko ni lazima kirushwe na hasa picha zinazoudhi;

7.5 Kamati imeona kuwa maelezo ya **Global TV** kuwa walitangaza habari hiyo kwa sababu ilitangazwa na vyombo vingine na hawakupokea malalamiko kutoka kwa wasikilizaji/watazamaji hayana msingi wo wote kwa sababu wanatakiwa kuzingatia Sheria, Kanuni na masharti ya leseni yao hata kama hawajalalamikiwa na hata kama kosa limefanywa na vyombo vingine pia;

7.6 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Global TV** imetenda makosa ya kuchapisha picha za mnato na kutangaza maudhui yasiyo na lugha ya staha na yenye kushabikia vitendo vya mahusiano ya kimapenzi ya jinsia moja kama ilivyotathiminiwa hapo juu na kama ambavyo wamekiri wenyewe, Kinyume na Kanuni Na. 5(1) (a) na (b), 7(1) (a) na (b) na 12 (b) za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018.

## 8.0 USHAURI WA KAMATI KWA GLOBAL TV.

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Global TV** kuimarisha usimamizi wa vipindi vyao ili kuepuka uvunjaji wa Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji wa Habari;

Pia, **Global TV** wanashauriwa kuhakikisha wanawapatia wasimamizi wa maudhui na watangazaji wao mafunzo ya mara kwa mara ya Uandishi na Utangazaji wa Habari ili kuwajengea uwezo zaidi wa kuepuka kutenda makosa.

## 9.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na **Global TV**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Global TV** kupitia chaneli yake ya YouTube wamekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Mitandaoni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **Global TV:**

1. Wanapewa Onyo Kali;
2. Wanatozwa faini ya **Shilingi Milioni Saba (TZS. 7,000,000.00)** tu, itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA);

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam leo tarehe **01 Julai, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

.............................................................
**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**.....................................
2. **Derek Kaitira Murusuri**.......................................
3. **Jacob Gregory Tesha**..........................................